JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

SHULE YA SEKONDARI KIBORILONI

Email kiborilonisecschool@gmail.com

SIMU: 0763318438

0674057317

0766423838

S.L.P 441, MOSHI

Tarehe ……/ 01 / 2021.

Kumb.Na. KBSS/SEL/F.1-2021/VOL.1/01

MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI

……

S. L. P. ……

……..

YAH. MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIBORILONI WILAYA YA MOSHI MJINI MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021.

1. **UTANGULIZI.**
   Nina furaha kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Kiboriloni mwaka 2021.
   Shule ipo umbali wa Km 5 Mashariki mwa mji wa Moshi. Usafiri unapatika kwa kutumia mabasi / daladala zinazofanya safari zake kuelekea Mjohoroni na kushushiwa kituo cha shule – Kiboriloni kwa nauli ya shilingi 200/= kwa mwanafunzi.

   Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11 / 01 / 2021**, mwanao anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **04 / 01 / 2021**, asubuhi **saa 1 : 30 asubuhi** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18 / 01 / 2021** baada ya siku saba **(7).**

2. **Mambo ya kuzingatia**
   - **2.1 Sare za shule**
     Sare ya shule hii kwa kidato cha kwanza ni rangi ya kitambaa kilichoambatitanishwa kwa wavulana na wasichana na maelekezo ya mshono yameelezwa vyema.
   - 2.2 Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu
   - 2.3 Chakula cha wanafunzi wa kutwa kama ilivyoelekezwa katika fomu ya kama ya chakula iliyoambatanishwa hapa, nauli ya kwenda na kurudi yumbani pamoja na matibabu (Mwanafunzi awe na kadi ya matibabu ya NHIF au TIKA)
   - 2.4 Picha passport size 2 za mwanafunzi
   - 2.5 Mahitaji mengine ya kibinadamu kama yapo.
3. **Sheria na kanuni muhimu za shule hii**
   Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

3.1 Ukiwa mwanafunzi wa shule ya Sekondari Kiboriloni utapaswa kufanya yafuatayo:

I. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
II. Mahudhurio mazuri na kuwahi katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ni la jambo lazima na kipaumbele sana. **Thamini matumizi ya muda.**
III. Kushiriki kwa makini kufanya mazoezi yote utakayopewa.
IV. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
V. Kutunza usafi wa mwili, nywele, mavazi na mazingira ya shule kwa ujumla.
VI. Kuvaa sare sahihi ya shule wakati wote unapokuwa shuleni.
VII. Kuzingatia na kuheshimu ratiba ya shule wakati wote na
VIII. Kutunza mali za umma, binafsi na za mwanafunzi mwenzako shuleni
IX. Kujua na kuimba wimbo wa shule,taifa na wa uzalendo kikamilifu.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Kupata au kusababisha mimba, kushiriki kutoa ama kuharibu mimba ndani na nje ya shule
5. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, kokaine, mirungi, kuberi n.k
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, picha ya rais, katiba ya Jamhuri nk
9. Kuoa au kuolewa
10. Kubainika kutembelea nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni
11. Kushirikimatendo ya uhalifu, siasa na matendo yanayovunja sheria za nchi
12. Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kujiua
13. Kugoma, kuchoche na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
14. Kukataa adhabu kwa makusudi
15. Kumiliki, kukutwa ukimiliki au kutumia SIMU ya mkononi ama vifaa vinavyohusiana na simu akiwa kwenye eneo la shule. Kukutwa na vifaa vya umeme shuleni bila taarifa.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

a) ''Medical Examination Form'' ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KIBORILONI SEKONDARI.

P.S. MWANGA.
MKUU WA SHULE

SARE ZA SHULE

Sare za shule zitashonwa na wazazi wenyewe

WAVULANA

- Suruali 2 na mashati meupe (02) ya mikono mifupi

- Sweta 1 rangi ya **" aqua blue"**

- Soksi nyeupe pea mbili (02)

Suruali za wavulana zifike kwenye kiatu na chini ziwe na upana usiopungua inchi 17 hadi 18.

Mwanafunzi akishona suruali inayobana maaarufu kama **KIBAMBA** hatapokelewa shuleni.

WASICHANA

-Sketi 2 na mashati meupe (02) ya mikono mifupi

-Sweta 1 rangi ya **" aqua blue"**

- Soksi nyeupe pea mbili (02)

Sketi za shule zina rinda box moja mbele na nyuma na marinda mawili upande wa kushoto na kulia ziwe na belti ya inchi moja na nusu na urefu wa sketi ifike kwenye kiatu.

NB: Pamoja ya fomu hii shule imeambatisha/ambatanisha sampuli ya kitambaa cha sketi,suruali na sweta kwa kidato cha kwanza 2021.

KWA WANAFUNZI WOTE

i. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga kwa kamba visiwe na kisigino kirefu na visiwe na mapambo. Viatu vya plastic havitaruhusiwa.

ii. Soksi ya rangi nyeupe zisiwe na mapambo wala maandishi.

MAHITAJI YA MASOMO

1. Begi la shule lisilo na mapambo wala maandishi.

2. Madaftari makubwa 14 (counter books quire 2 au 3).

3. Kalamu za wino na penseli za kumtosha

4. Mkebe wa mahesabu "Mathematical set"

TANBIHI

Shule haina uwezo wa kuwapa wanafunzi wote vitabu vya kutosha vya rejea,hivyo unasisitizwa kumnunulia wanao vitabu vya rejea ili kuwezsa kumsaidia kitaaluma. Pata orodha shuleni.

MAHUDHURIO

1. Wanafunzi wanatakiwa kuwepo shuleni muda wote wa masaa ya shule

2. Wanafunzi wanatakiwa kuwahi na kushiriki katika shughuli zote za shule kama usafi wa mazingira ,shughuli za uzalishaji mali,michezo nk.ATAKAYECHELEWA AU KUKOSA ATAADHIBIWA AU ATARUDISHWA NYUMBANI.

3.Wanafunzi wanatakiwa kuitika mara moja na kukimbia atakiwapo,asikiapo kengele au mwito mwingine wowote.

4.Ni lazima mwanafunzi awahi shule katika tarehe zilizopangwa mwanzoni mwa kila muhula au baada ya mapumziko ya aina yoyote.

TAHADHARI.

Ruhusa ya kutokuwepo shuleni siku moja au zaidi ni lazima itoke kwa mkuu wa shule au makamu wake.Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye atakaye husika kumwombea ruhusa na sio mtu mwingine.

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

SHULE YA SEKONDARI KIBORILONI S. L. P 441 MOSHI, SIMU 0763318438

FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI YA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

A. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi (la mtihani wa darasa la saba) ……..
Tarehe ya kuzaliwa (ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa) …….
Mahali pa kuzaliwa (Wilaya, Mkoa) ……
Uraia: Mtanzania / Si Mtanzania ……..
Shule ya msingi alipohitimu darasa la saba ……..
Namba ya mtihani wa Taifa aliyoitumia kufanya mtihani wa darasa la saba ……

B. <u>KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE:</u>

Mimi …….. Nakubali nafasi ya kidato cha……mwaka

Niliyopewa katika shule ya Sekondari Kiboriloni.
Ninayakubali masharti na kuwa nitatii sheria za shule zilizoko na zile zitakazotolewa kwa muda wote wa masomo yangu.
Naahidi kuwa nitawaheshimu na kuwatii waalimu, wanafunzi na wafanyakazi wasio waalimu wote kama walezi wangu muda wote nikiwa mwanafunzi hapa shuleni.
Ninaahidi kuwa nitawatii wale wote watakaoteuliwa au kuchaguliwa kuwa viongozi wangu kwa mujibu wa sheria.
Ninaahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mwaminifu na pia nitajielimisha kwa nguvu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu.
Natambua kuwa nikikiuka ahadi hizi nitapoteza nafasi yangu hapa shuleni
JINA LA MWANAFUNZI ……..
SAINI YA MWANAFUNZI ……..

JINA LA MZAZI / MLEZI ……..
SAINI YA MZAZI / MLEZI ……Namba ya simu.....

C. TAARIFA ZA SERIKALI ZA MITAA ANAKOTOKEA MWANAFUNZI.

MTAA …….. KATA …….. WILAYA ……
JINA MWENYEKITI WA KITONGOJI / MTAA ……
NAMBA YA SIMU …… SAHIHI NA MUHURI ……..
JINA LA MTENDAJI WA KATA ……..
NAMBA YA SIMU …… SAHIHI NA MUHURI ……

NB. Tafadhali mzazi / mlezi fika shuleni siku ya Alhamisi ya tarehe 21/ 01 / 2021, saa 3 : 00 asubuhi, kwenye kikao cha wazazi ili tujadiliane kwa pamoja mambo yanayohusu watoto wetu.

PRESIDENT OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

KIBORILONI SECONDARY SCHOOL BOX. 441, MOSHI. PHONE 0763318438

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by Medical Officer from a recognized Governmental Hospital.

Full Name of the Student …… Sex: ……..

Please examine the student named above who has been selected to join this school for his / her fitness as a student in the following areas:

1. Eye sight ……
2. Hearing …….
3. Specimen
   - (i) Stool ……..
   - (ii) Urine …….
   - (iii) Blood ……..
4. Asthma / Tuberculosis ……..
5. Pregnancy ……
6. Other diseases ……..
7. Chest ……
8. Abdomen ……
9. Spleen ……..

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by the medical Officer)

I have examined the above and considered that he / she is physically FIT / NOT FIT as a student.

Date …… Signature ……..

Station …….. Designation …….

OFFICIAL STAMP

OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI
SHULE YA SEKONDARI KIBORILONI S. L. P. 441, MOSHI SIMU 0763318438
FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MZAZI / MLEZI YA KUKUBALI KUMSIMAMIA MWANAFUNZI KUTIMIZA SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA.

	JINA LA KWANZA	JINA LA KATI	UKOO	UMRI	KAZI	YUPO HAI	SIMU
BABA							
MAMA							

Anwani ya nyumba; Kijiji / Mtaa unakoishi …… Kata ……
Wilaya …….. Mkoa ……..
Anwani ya nyumbani, S. L. P. …….. Simu ……..

NDUGU WA KARIBU WALIOIDHINISHWA NA MZAZI / MLEZI PALE AMBAPO MZAZI / MLEZI HATAKUWEPO KUFUATILIA TARATIBU ZA SHULE.

S/N	JINA KAMILI	UHUSIANO NA MWANAFUNZI	KAZI YAKE	SIMU
1.				
2.				

UTAMBULISHO WA PICHA

PICHA	PICHA	PICHA	PICHA
BABA / MLEZI	**MAMA / MLEZI**	**NDUGU WA KARIBU - 1**	**NDUGU WA KARIBU - 2**
SAHIHI……	**……**	**……**	**……**

AHADI YA MZAZI / MLEZI
Mimi …… mzazi / mlezi wa mwanafunzi ……
Kidato cha …… mwaka …… ninakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa kwa kipindi chote mwanangu atakachokua katika shule ya Sekondari Kiboriloni.
Pia nahidi kuwa nitashirikiana na walimu kumlea mwanangu katika maadili yanayotakiwa awapo shuleni ama nyumbani na kumfuatilia katika kujua maendeleo yake kitaaluma.
Naahidi kuchukua matokeo yake kila mwisho wa muhula, kujadiliana na mwanangu mafanikio au changamoto zinazomkabili kitaaluma na hatimaye kufika shuleni kuashirikisha uongozi wa shule au na walimu wanaomfundisha mwanangu.

MUNGU NAOMBA NISAIDIE KUTIMIZA WAJIBU WA MALEZI KWA MWANANGU.